BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA
# TNMC HABARI
Jarida la Mwezi
Februari, 2024
Toleo N0. 005
HALIUZWI
www.tnmc.go.tz
@tnmchabari

# Prof Nagu: Marufuku Matumizi ya Simu Wakati wa Utoaji Huduma.

## Ni Kwa Watumishi wa Afya Katika Hospitali na Vituo vya Afya Nchini.

Habari UK 01




## Makamu wa Rais Amtunuku Tuzo Afisa Muuguzi Mwandamizi wa TNMC Bi. Salome Kassanga

Tuzo hiyo muhimu na ya heshima kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) Habari UK 03.

## Waziri Nape Atunuku Cheti Cha Pongezi Kwa TNMC

ikiwa ni kutambua mchango wake wa kudhamini Mkutano wa watayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa umma ulioandaliwa na TBC. Habari UK 06.

# BODI YA WAHARIRI




## MWENYEKITI

**Bi. Agnes Mtawa**

## MHARIRI

**Mwakapiso Ndimmyake**

## WARATIBU

**Irene chelewa na Rose Mhando**

## MSANIFU JARIDA

**Ezekiel M Nyalusi**


**S.L.P 1736 DODOMA Simu:0737-96-26-91**

@tnmchabari www.tnmc.go.tz Info@tnmc.go.tz

# Mganga Mkuu wa Serikali Apiga Marufuku Matumizi ya Simu Wakati wa Utoaji Huduma.



*Wauguzi na Wakunga wakiapishwa katika Mahafali ya 10 ya Kitaaluma ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) Jijini Dodoma.*

***Na Ndimmyake Mwakapiso.***

JMganga Mkuu wa Serikali Prof. Tunaini Nagu, amepiga marufuku matumizi ya simu za mkononi kwa watumishi wa Afya wanapokuwa kazini na kuwaagiza waganga wafawidhi katika Hospitali zote nchini kusimamia utekelezaji wa katazo hilo.

Kiongozi huyo ambaye ni msimamizi mkuu wa wanataaluma wote katika sekta ya Afya, ametoa agizo hilo alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya 10 ya Baraza la Uuguzi na ukunga yaliyofanyika Jijini Dodoma 23 Februari 2024, ambapo jumla ya wauguzi na wakunga 2,099 walisajiliwa na kupewa Leseni.

*"Hapo nyuma kama wiki mbili au tatu zilizopita, niliongelea masuala ya simu na nilisema marufuku kutumia simu, naomba nirudie ile marufuku yangu, marufuku kutumia simu tukiwa tunatoa huduma, naomba niwakumbushe mazingira ya Hospitali ni ya infection (maambukizi) namna bora ya kujikinga ni kunawa mikono lakini simu mara umeweka kwenye kitanda cha mgonjwa mara umeweka mahali fualani unabeba kila aina ya vimelea."*

*Tunafanya hivi ili kuzuia maambukizi kutoka kwa mgonjwa mmoja Kwenda kwa mwingine lakini pia kwenu ninyi maana simu huwezi kuiosha, ukienda mapumnziko ya chai tumia simu yako, ukienda nje ukiomba nafasi tumia simu zako naomba pia niwaagize wafawidhi wote, waganga wafawidhi katika hospitali zetu zote kuhakikisha wanasimamia hili, tukienda kwenye hospitali za private(binafsi) hili linasimamiwa vizuri"* alisema

Katika hatua nyingine Mganga Mkuu amewataka wauguzi na wakunga kuwa na mawasiliano mazuri na wateja wanapofika vituoni kupata huduma.

*"Tunalalamikiwa sana, lugha tunazotumia kwa wateja wetu ni lugha zisizojali umri wala utu ni lugha zisizo na staha, naomba lugha zetu tuziangalie ziwe lugha za upendo na kutia Moyo"*
*"Lakini pia, kwa tamaduni zetu tunaweza kusema leo ndio mmemaliza jando na unyago katika taaluma hii ya uuguzi na ukunga Tanzania, kwa kufikia hadhi ya kuorodheshwa rasmi kuwa wauguzi na wakunga hivyo, tembea yako, vaa yako Mwenendo wako na hata matumizi yako ya Mitandao ya kijamii, ilete taswira ya Muuguzi na Mkunga"*

Katika hatua nyingine Prof. Nagu, amewapongeza wauguzi na wakunga kwa kufanikiwa kupunguza kwa asilimia kubwa vifo vitokanavyo na uzazi, pamoja na vifo vya watoto chini ya umri wa miaka 05 na kuwataka kuongeza juhudi katika kupunguza vifo vya Watoto wenye umri wa chini ya mwezi mmoja kwa kuwa takwimu zinaonesha katika eneo hilo hali si nzuri.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake, miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kuratibu na kuendesha Mitihani kwa wanataaluma kabla ya kusajiliwa na kupewa leseni ya kufanya kazi kama Wauguzi na Wakunga hapa nchini na Mitihani hii hufanyika kwa wanachuo waliohitimu katika vyuo mbalimbali ndani na hata nje ya Nchi.

# TNMC Yatoa Mafunzo ya Sheria na Maadili kwa wauguzi, wakunga Mkoani Geita.



*Wauguzi na wakunga Mkoani Geita wakifuatilia kwa makini Mafunzo ya Maadili na Sheria ya Uuguzi na Ukunga yaliyoandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.*

***Na Ezekiel Nyalusi***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) liliweka kambi ya siku sita Mkoani Geita kwa lengo la utoaji Mafunzo ya Maadili na Sheria ya Uuguzi na Ukunga kwa wauguzi na wakunga katika Halmashauri zote za Mkoa humo.

Ziara hiyo ya Mafunzo ni ya kawaida kwa mujibu wa ratiba za Ofisi ya Msajili, inalengo la kutoa Elimu ya Maadili na Sheria kwa wauguzi na wakunga ili waendelee kutoa Huduma kwa kuzingatia Maadili, Sheria, kanuni na taratibu hivyo jamii iweze kupata Huduma iliyo bora na Salama.

Akitoa Mafunzo hayo katika Halmashauri sita za Mkoa wa Geita, Msajili wa Baraza Bi. Agnes Mtawa, amewapongeza wauguzi na wakunga Nchini kwa utoaji Huduma bora kwa jamii, huku akibainisha kuwa, takribani asilimia 60 hadi 80 ya watoa Huduma za Afya Nchini, ni wauguzi na wakunga, hivyo ni vyema wakapata Mafunzo hayo ili kuendelea kuboresha zaidi Huduma za Afya Nchini.

Kwa upande wake Mwanasheria wa Baraza Wakili George Shilla, aliwasisitiza wauguzi na wakunga kujitokeza katika vituo vilivyopangwa kwa ajili ya Mafunzo hayo ili kuijua vyema Sheria ya Uuguzi na Ukunga inaiongoza Taaluma hiyo hapa nchini.

Naye Bi. Mwajuma Mutabazi, ambaye ni Muuguzi Mbobezi kutoka Baraza amesema, ili kuwa Muuguzi na Mkunga mzuri ni vyema kuzingatia Maadili ya taaluma huku ukitanguliza Utu katika utoaji Huduma.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa Mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010 na Kanuni zake, kwa lengo la kusimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga, ili kuhakikisha jamii inapata huduma za Afya zilizo bora na Salama.

# Makamu wa Rais Amtunuku Tuzo Afisa Muuguzi Mwandamizi wa TNMC Bi. Salome Kassanga



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, akimkabidhi tuzo Bi. Salome Kassanga, ambaye ni Mtumishi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) Tuzo hiyo imetolewa visini Zanzibar.*

***Na Ndimmyake Mwakapiso***

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango, amemkabidhi tuzo Bi. Salome Kassanga, ambaye ni Mtumishi wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kufuatia utumishi wake kama Muuguzi Kiongozi wa Kwanza wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ya Jijini Dar es Salaam na kutoa mchango chanya katika Taasisi hususani katika matibabu ya upasuaji wa magonjwa ya Moyo kwa jamii.

Tuzo hiyo muhimu na ya heshima kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imeandika historia ya kipekee kwa Afisa huyo ikimtambua kama Muuguzi kiongozi mwanzilishi wa huduma za upasuaji wa magonjwa ya Moyo hapa nchini, imetolewa mnamo tarehe 09.02.2024 Visiwani Zanzibar wakati wa ufunguzi wa mkutano wa kimataifa wa magonjwa ya Moyo.

Akisimulia kuhusu historia iliyochangia kutunukiwa tuzo hiyo, Bi. Salome, ametanabaisha kuwa; alishiriki kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa Jengo la upasuaji la Hospitali ya JKCI na mnamo mwaka 2012 huduma za upasuaji wa moyo zilianza, alihudumu kupitia cheo cha Mkuu wa Idara ya Uuguzi hadi mwaka 2017 alipohamishiwa Mkoani Dodoma katika Hospitali ya kanda ya Benjamini Mkapa.

*"Nilipohamishiwa hospitali ya Benjamini nilitumikia cheo cha Mkurugenzi wa Uuguzi na Ukunga ambapo hospitali ikiwa katika hatua za awali za uanzishwaji wa huduma za matibabu mbalimbali ikiwemo upasuaji wa moyo bila kufungua kifua, nilihudumu hadi 2021 kabla ya kuhamishiwa katika Taasisi ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), nimeendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa watumishi wa vyumba vya upasuaji katika Hospitali mbalimbali hapa nchini.*

*Mafunzo hayo yameleta matokeo chanya na yenye tija kwa wagonjwa wetu kwa kupata huduma zilizo Bora na salama wanapofanyiwa upasuaji ikiwa ni kutimiza lengo kuu la uwepo wa TNMC"*

Bi. Salome Kassanga, Afisa Muuguzi mbobezi katika chumba cha upasuaji wa kawaida na Moyo.(general and open heart surgery) pia amewahi kutumikia cheo ha uongozi kama Mkuu wa Jengo la upasuaji (Operating Theatre Manager) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kabla ya kujiunga na mafunzo ya upasuaji wa Moyo huko ughaibuni nchini India.

# “Wasajili Simamieni Maadili Katika Kada ya Afya” - *Katibu Mkuu Jingu*




*Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, akizungumza na Wasajili wa Mabaraza ya kitaaluma, katika kikao kazi kilichofanyika Februari 02.2024 Jijini Dodoma.*

***Na Mwandishi wetu;***

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, amewaagiza Wasajili wa Mabaraza na Bodi za kitaaluma zilizo chini ya Wizara ya Afya, kuimarisha na kusimamia mifumo ya Maadili ya kitaaluma na ya kazi kwa watumishi wa kada ya Afya, kwa kufika katika maeneo yao ya kazi ili kuzuia matatizo ya uvunjifu wa Maadili kwa watumishi wa Umma na kuhakikisha jamii inapata Huduma bora na Salama.

Katibu Mkuu, ametoa rai hiyo Februari 02.2024 alipofanya kikao kazi na Wasajili wa Mabaraza, Wasajili, wasaidizi wa Mabaraza na Bodi za ushauri zinazosimamia taaluma na wanataaluma wa kada mbalimbali za Afya ikiwa ni pamoja na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

*“Nendeni field, tuwe na mikakati ya kuwafikia watu wetu, fuatilieni namna ambavyo wanafanya kazi Kuna baadhi ya wataalamu wetu ni watukutu, hawazingatii Maadili kama vile kutibu kinyume na tiba inayotakiwa, kutoa siri za wagonjwa, lakini pia tuimarishe Mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wataalamu wetu wakiwa kazini (CPD), tusisubiri matatizo yatokee, tuwe makini na wepesi wa kushughulikia mambo kabla hayajaharibika”.* alisisitiza Katibu Mkuu Jingu.

Akizungumzia suala la ugatuaji wa Madaraka, Katibu Mkuu Dkt. Jingu, amewataka Wasajili kugatua Madaraka kwa wasimamizi wa ngazi za Mikoa RNO na RMO ili kupata usimamizi wa karibu katika kusimamia taaluma na wanataaluma, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo ili wawe na weledi na maarifa sahihi ya kutekeleza majukumu waliyokasimiwa kwa ufasaha.

Akizungumzia suala la Mabaraza na Bodi za ushauri kujulikana na Wananchi, Katibu mkuu alisisitiza kwamba Mabaraza yatumie vyombo mbalimbali kujitangaza ili yajulikane na jamii.

*“Nasisitiza, tujitangaze ili tufahamike, tuhakikishe kuwa Mabaraza yetu yanajulikana kwa Umma, tujitangaze kwa kufafanua majukumu yetu ili Wananchi watufahamu na wanapokuwa na jambo wajue wapi pakwenda”* alitanabaisha.

Akihitimisha Hotuba amesema, pamoja na Mabaraza hayo kuwa ni Mamlaka za kisheria, hazitakiwi kuleta changamoto kwa wawekezaji waliowekeza au wanaotaka kuwekeza katika sekta ya Afya kwani Serikali imekuwa ikihamasisha uwekezaji katika sekta hiyo, hivyo utekelezaji wa majukumu yao usiwe na usumbufu, mfano kila Baraza Kwenda kwa wakati wake kukagua, bali Mabaraza yote mjipange na kwenda kwa pamoja kwenye kaguzi na kutoa mrejesho kwa wakati.

# Bilioni 899.4 Kuajiri, Kujenga Uwezo kwa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii.



*Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdori Mpango, katika Uzinduzi wa Mpango wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii uliofanyika katika kituo cha Mkutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar Es Salaam, Januari 31, 2024*

***Na Mwandishi wetu;***

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 899.4 kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kuajiri na kuwajengea uwezo Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wapatao 137,294 katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

Hayo yamesemwa na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdori Mpango, Januari 31, 2024 kwenye Uzinduzi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii uliofanyika katika kituo cha Mkutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere Jijini Dar Es Salaam.

*“Utekelezaji wa Mpango huo utafanyika katika kipindi cha Miaka Mitano kwa awamu ambapo mwaka wa kwanza 2023-2024 zaidi ya wahudumu 28,000 watafikiwa na baadaye wastani wa wahudumu 27,324 kila mwaka kwa kipindi cha miaka Minne mfululizo kuanzia mwaka 2024-2025 hadi 2027-2028.”* Amesema Makamu wa Rais Dkt. Mpango.

Aidha, Dkt. Mpango, amezielekeza Wizara za Afya, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na na Mamlaka nyingine zinazohusika kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi madhubuti wa Mpango Jumuishi wa Huduma ya Afya Ngazi ya Jamii ili uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Dkt. Mpango, amewasihi viongozi wote wanaohusika katika ngazi zote kuhakikisha zoezi la kuwachagua wahudumu wa Afya ngazi ya jamii linafanyika kwa kufuata vigezo na taratibu zilizowekwa ili kupata wahudumu wenye sifa stahiki watakaotekeleza majukumu hayo na kuwataka watakaopewa jukumu la kutekeleza mpango huo, kujiepusha na vitendo vya upendeleo, Rushwa au ukiukwaji wa taratibu.

*“Wahudumu wa Afya mtakaopewa dhamana ya kutekeleza jukumu hili zingatieni Weledi na kujituma pamoja na kutoa rai kwa jamii kuupokea mpango huo na kuthamini huduma za wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii kwa kuwapa Ushirikiano wa kutosha ili kulinda na kuboresha Afya katika jamii.”* Amesisitiza Makamu wa Rais Dkt. Mpango.

# Waziri Nape Atunuku Cheti Cha Pongezi Kwa TNMC




*Mhe. Waziri Nape, akikabidhi cheti cha pongezi kwa Afisa wa Baraza Ndg. Nyalusi wakati wa ufunguzi wa Mkutano ulioandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania TBC jijini Mwanza*

***Na Ezekiel Nyalusi;***

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mtama Mkoani Lindi Mhe. Nape Nnauye, ametunuku cheti kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) ikiwa ni kutambua mchango wake katika kuistawisha sekta ya Habari na Mawasiliano kwa kudhamini Mkutano wa watayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa Umma ulioandaliwa na TBC.

Mhe. Nape, amekabidhi cheti cha pongezi wakati wa ufunguzi wa Mkutano ulioandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania TBC ukiwahusianisha watayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa Umma ambao ulifanyika Jijini Mwanza kwa siku tano kuanzia tarehe 18/02/2024 mpaka 23/02/2024 ambapo Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni sehemu ya wadhamini wa Mkutano huo.

Mkutano huo uliobebwa na kauli mbiu ya *"Vyombo vya Habari na Falsafa ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya 4R"* ikiwa na maana ya Mageuzi, Maridhiano, Usitahimilivu na Kulijenga Taifa kwa pamoja, ambapo kila Mtanzania anatakiwa kushiriki ujenzi wa Taifa, ambapo mada mbalimbali zinazohusu utayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa Umma zilitolewa.

*"Tumieni Mkutano huu kujifunza mambo Muhimu kwa ajili ya kuhabarisha Umma hasa matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii, ndio maana Serikali inaona kuna umuhim wa kila idara na Taasisi za Umma ziwe na Maafisa Habari ili kuupa Umma taarifa na hasa kujibu kero za wanajamii"* -Waziri Nape.

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kimeshiriki Mkutano wa Mafunzo wa watayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa Umma kupitia TBC ambapo Ezekiel Nyalusi Afisa Uhusiano TNMC, amepokea Cheti cha pongezi ya udhamini wa Mkutano huo kwa niaba ya Baraza.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya 2010, na Kanuni zake kwa lengo la kuhakikisha Huduma zitolewazo na wauguzi na wakunga zinaubora na salama kwa jamii.

# LIFAHAMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA (TNMC)

## SEHEMU YA SITA;
## MASHARTI KUHUSU NIDHAMU ZA WAUGUZI NA WAKUNGA



Msajili kupokea Malalamiko; Msajili, kwa niaba ya Baraza, atapokea malalamiko dhidi ya muuguzi au mkunga yeyote kuhusu kupoteza sifa za kutoa Huduma na kuwasilisha malalamiko hayo mbele ya Baraza kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kupoteza sifa za kutoa Huduma" maana yake ni sifa ya mtu kutoa Huduma imeathirika kwa sababu ya-

(a) Kukosa Maadili ya kitaaluma;
(b) Kukosa Umahiri;
(c) Kutiwa hatiani kwa kosa la Jinai;
(d) Afya yake ya viungo au akili haipo sawa;
(e) Uamuzi wa Bodi ya Kitabibu Tanzania au Mamlaka nyingine yoyote inayotoa leseni kwenye masuala ya Afya.
(f) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2) Maneno "kukosa maadili ya kitaaluma" yatamaanisha, lakini siyo kwa ukomo-
(a) Ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii au kanuni;
(b) Kushindwa kuzingatia vigezo, masharti, aumipaka ya leseni kama Muuguzi au Mkunga aliyesajiliwa au kuorodheshwa;
(c) Kumnyanyasa mteja kwa maneno, vitendo, kingono au kihisia;
(d) Kuwa na mgongano wa maslahi ambao unaathiri Mahusiano ya Mteja na mtoa Huduma;
(e) Kumshawishi mteja kubadili uamuzi wake, kumshawishi kupata aina ya Huduma ya Afya au hati ya uwakilishi wa kisheria;
(f) Kumtelekeza Mteja ambaye anahitaji Huduma;
(g) Matumizi mabaya ya dawa au mali zingine zinazomilikiwa na Mteja au Mwajiri;
(h)Kushindwa kutoa taarifa juu ya kukosa Umahiri, Uzembe au kosa la Maadili ya kitaaluma ya Mtumishi mwenzake ambaye vitendo vyake vinahatarisha Afya ya Mteja;
(i) Kushindwa kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na Utoaji wa taarifa za siri za Mteja;
(j) Kugushi kumbukumbu kuhusiana na uchunguzi au matibabu ya Mteja;
(k) Kushindwa kudumisha viwango vya Huduma na kanuni za Maadili ya kitaaluma; na
(l) Mwenendo wowote au kitendo chochote katika utoaji Huduma ambacho kwa kuzingatia Mazingira katika taaluma kitaonekana ni cha kuaibisha, kisicho cha kitaaluma au kitendo ambacho kitamdhuru Mteja.

(4) Kila lalamiko chini ya kifungu hiki litaambatishwa na maelezo ya maandishi ya mlalamikaji, au Mtu yeyote kwa niaba ya mlalamikaji au Mtu yeyote aliyeguswa na kitendo au mapungufu yaliyopelekea lalamiko.

(5) Bila kujali Masharti ya kifungu kidogo cha (4) Baraza linaweza, kwa azimio lake kuanzisha Uchunguzi wa awali juu ya muuguzi au mkunga iwapo likiridhika kuwa taarifa zilizopokelewa, zinatosheleza kufanyika kwa Uchunguzi wa awali. Sheria ya Uuguzi na Ukunga 15 (6) Isipokuwa kwa Malalamiko yaliyotokana na Makosa.

Itaendela katika toleo lijalo....

# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki Mwezi wa 02 mwaka 2024, baada ya kumaliza kazi yao hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi AMINA.



**JINA: EVARIST EDWARD KAYIMBA**
**KITUO :** Hospitall ya Rufaa - Tumbi.
**MKOA :** Pwani
**WILAYA :** Kibaha DC



**JINA: VERONICA KADAMA**
**KITUO :** Hospitall ya Rufaa.
**MKOA :** Dar es Saalam
**WILAYA :** Temeke



**JINA: MARY NYENGO**
**KITUO :Zahanati**
**MKOA :** Songea
**WILAYA :** Tunduma mjini.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

## TAARIFA KWA UMMA

## UTOAJI WA VYETI VYA USAJILI NA LESENI BAADA YA MAHAFALI YA 10 YA TAREHE 23 FEBRUARI, 2024.

**Dodoma, 25 Februari, 2024.**

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga waliofanya Mtihani wa Usajili na Leseni tarehe 29.12.2023 na kufaulu na hawakuweza kuhudhuria kwenye Mahafali ya 10 ya Kitaaluma kwa sababu mbalimbali kuwa, wanatakiwa kufika Ofisi ya Msajili, Jengo la Kambarage, Barabara ya Mkapa, Ghorofa ya 5, kuanzia tarehe **08 Machi, 2024** ili kuchukua vyeti na Leseni ambavyo vitatolewa kuanzia **Saa 02:00 asubuhi hadi 10:00 Jioni** kwa siku za kazi tu.

Aidha, Mhitimu atatakiwa kuja na **kitambulisho** cha NIDA au mpiga kura au Leseni ya Uuguzi na Ukunga ambacho kitatumika kama utambulisho wakati wa kuchukua cheti na leseni.

**Ikumbukwe kuwa vyeti na Leseni vitatolewa kwa Muhitimu husika tu na hairuhusiwi kumchukulia Mtu**.

Kwa taarifa Zaidi tafadhali piga simu namba:- ***0628583390, 0682896529, 0758589706.***

Nawatakia utekelezaji mwema.

**Imetolewa na:**

Agnes Mtawa
**MSAJILI**

Jengo la Kambarage Tower, Ghorofa ya 5, Barabara ya Benjamini Mkapa, S.L.P 1736, DODOMA Simu: +255262966061/62/63, +255737 962 691, Barua pepe: info@tnmc.go.tz, Tovuti: www.tnmc.go.tz

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA
TANZANIA TOLEO NO 05

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA